HOTUBA

KILELE CHA MAADHMISHO YA WIKI YA ELIMU

WILAYA YA KINONDONI

MGENI RASMI: NAIBU MEYA WA MANISPAA YA KINONDONI

TEREHE: 12/05/2017

Katibu Tawala wa Wilaya,
Mkurugenzi Manispaa ya Kinodnoni,
Wahe: Madiwani Manispaa ya Kinondoni,
Wakuu wa Idara na Vitengo Masnispaa ya Kinondoni,
Watendaji wa Kata na Maafisa Elimu Kata,
Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari,
Walimu Wote,
Wazazi,
Wadau wote wa Elimu kutoka taasisi mbalimbali na
Wanafunzi wote

Awali ya yote naomba kuchua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo kwa ajili ya kuhitimisha shughuli zetu za Elimu ambazo tumekuwa tukizifanya kuadhinisha juma la Elimu ambapo leo tunafikia tamati.

Wiki ya Elimu au Juma la Elimu hufanyika kila mwaka kwa lengo la kushirikiana kwa pamoja sisi tukiwa Wadau wa Elimu kutathmini

maendeleo ya Elimu kwa Mwaka Mzima, kujikosoa tulipojikwaa na kuweka mikakati kabambe ya kutuwezesha kusonga mbele zaidi. Wakati huu ni muhimu sana tukaa pamoja kama tulivyofanya leo na kuwa na tafakari ya pamoja. Maadhimisho haya kama tulivyoambiwa na Mkurugenzi wa Manispaa yalianza kwa shule zetu kufanya shughuli mbalimbali za kielimu katika ngazi ya shule na kata. Baadaye tarehe 19/04/2017 tulifanya kikao cha Wadau wa Elimu katika Wilaya ya Kinondoni kwenye ukumbi wa King Solomon ambapo wadau walipata siku nzima ya kutafakari kwa pamoja mafanikio na changamoto zinazokabiri utoaji wa elimu katika wilaya yetu, maoni na mapendekezo ya wadau yalitolewa kwa kina ambapo kupitia mapendekezo hayo Manispaa inaandaa Mkakati wa Maendeleo ya Elimu wa Miaka mitatu 2017/2018 hadi 2019/2020. Hili ni jambo kubwa sana, tunawaomba Viongozi wa Manispaa kuharakisha utayarishaji wa Mkakati huo ili Mwezi Julai 2017 utekelezaji wake uanze.

Tuamembiwa pia kupia Wiki ya Elimu tarehe 24/05/2017 wenzetu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzani kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni walitoa Madaktari kwa ajili ya uchunguzi na ushauri kwa wanafunzi na Walimu wetu wa magonjwa ya ngozi, moyo na kisukari. Katika zoezi hili jumla ya wanafunzi 546 na Walimu 76 walihudumiwa. Katika kutoa huduma hii ilibainika wazi kuwa baadhi ya wazazi hawajishirirki kikamili kufuatilia afya za watoto wao. Baadhi ya watoto walikutwa na changamoto kubwa za kiafya. Nichukue fursa hii kuwaomba Wazazi wote ambao walipata taarifa kutoka

kwa Walimu kuhusu matokeo ya uchunguzi wa afya za watoto wao kufuatilia matibabu hayo ipasavyo. Aidha nitoe wito kwa Wazazi wote Manispaa ya Kinondoni kuwa na utaratibu wa kuchunguza afya za watoto wao mara kwa mara na kutoa kipaumbele cha kwanza kwenye matibabu yao. Mafanikio hayo pia na mchango mkubwa wa uongozi wa Manispaa ya Kinondoni likiwemo Baraza la Madiwani na Watendaji wanaoongozwa na Mkurugenzi wa Manispaa. Hawa pia tutatambua juhudi zao.

Ndugu Wadau wote wa Elimu; Leo sote tumeshiriki katika maonesho ya kitaaluma, hapa tumeona shughuli mbalimbali za ujifunzaji zinazoendelea katika shule zetu za msingi na sekondari katika Manispaa ya Kinondoni. Tumeona shule za Serikali na Zisizo za Serikali. hiyo pia ni Sehemu ya Maadhimisho haya. Aidha tumnaweza kuona wingi wa tuzo zilizopo ambazo pia tutawazawadia wanafunzi, walimu na shule zilizofanya vizuri katika mitihani ya kitaifa mwaka 2016. Tutapata fursa ya kutambua juhudi za walimu na wanafunzi wetu jinsi walivyo pambana kufundisha na kujifunza ili kuinua taaluma katika shule husika. Lakini mafanikio ya shule yoyote hayawezi kutenganishwa na Uongozi wa shule husika, kwamaana ya Bodi na Kamati za Shule pamoja na jamii husika. Hawa wote leo tutawapongeza.

Lakini pia tumepata fursa za kuona vikundi vya Sanaa za maonesho kama nyimbo, ngonjera na ngoma kutoka katika shule zetu za msingi na sekondari. Hii inaonesha namna ambavyo katika shule zetu shughuli za kiutamaduni zinavyofanyika. Nichukue fursa hii kuwapongeza walimu na wanafunzi wote walishiriki katika maandalizi ya vikundi hivi vilivyotuburudisha hapa leo.

Ndugu Wadau wote wa Elimu; Sote tunafahamu kuwa kauli mbiu ya maadhimisho ya juma la Elimu kwa Mwaka huu ni '**Uwajibikaji wa Pamoja kwa Elimu Bora'**. Kauli mbiu hii inatuhimiza wote kwa pamoja kushirikiana katika uendeshaji wa elimu yetu nchi. Jukumu la maendeleo ya elimu yetu ni letu sote. Elimu bora ni jukumu la Wanafunzi wenyewe, Walimu, Wazazi, Serikali, Wadau mbalimbali wa Elimu zikiwemo taasisi zisizo za kiserikali na Jamii kwa ujumla. Kupitia kauli mbiu hii kila mmoja wetu anakumbushwa kutimiza wajibu wake. Mawazo kwamba jukumu la maendeleo ya Elimu ni laSerikali tu siyo sahihi. Hivyo napenda kutumia siku hii kuwahamasiha Wazazi wote kusimamia maendeleo ya wattoto wao kwa kufuatilia ujifunzaji wao wa kila siku uliofanyika shuleni na kuhakikisha kuwa kazi walizopewa shuleni wakafanye nyumbani wanazifanya ipasavyo. Aidha ni wajibu wa Wazazi pia kukagua kazi za watoto wao kuona kama wanajifunza ipasavyo shuleni na pale wanapoona kuna mapungufu basi wawasiliane na walimu wa madarasa na Wakuu wa shule husika. Wazazi tusiwaachie Walimu tu. Wazazi pia wana majukumu mengine yaliyoainishwa kwenye Waraka wa Elimu Na. 6 wa Mwaka 2015**kuhusu utekelezaji wa Elimu**

Msingi Bila Malipo, ambayo ni pamoja na kugharamia chakula cha watoto wao wawapo shuleni kwa shule za Msingi na Sekondari za Kutwa, gharama za matibabu, sare za shule, na Usafiri kutaja vichache. Hivyo Wazazi naomba kuwasihi sana kuhakikisha mnatimiza wajibu wenu kwa upande wenu ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wawapo shuleni na wawapo nyumbani wanajifunza ipasavyo.

Wadau wa Elimu na Jamii kwa ujumla wanalo jukumu la kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya shule zetu ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya shule, ulinzi wa maeneo ya shule yasivamiwe na wananchi wenye nia mbaya na kutatua kero mbalimbali zinazobainika kukwamisha maendeleo ya elimu shuleni.

Kwa upande wa Serikali mpaka sasa kazi kubwa imefanyika; kwa mfano, tayari kila mwezi Serikali hutoa Zaidi ya Billion 18 kugharamia elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari za Serikali kote nchini, utengenezaji wa madawati kwa shule za msingi na sekondari kwa wilaya yetu umekamilika ambapo kila mwanafunzi sasa anakaa kwenye dawati. Ujenzi wa vyoo na vyumba vya madarasa unaendelea ambapo Serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa lakini upungufu ni mkubwa sana. Kwa mfano upo upungufu wa vyumba vya madarasa 908 kwa shule za Msingi na Madarsa 134 kwa shule za Sekondari, pia upo upungufu wa vyoo matundu 2742 kwa shule za Msingi na Matundu 475 kwa shule za Sekondari. Changamoto hii

inatuhimiza Wadau wote wa Elimu ikiwemo jamii yenyewwe kushikiriki kikamilfu katika utatuzi wa changamoto hii na zingingine ambazo sijazitaja. Tusikae pembeni kuisubiri Serikali tu, Serikali ina majukumu mengi kwa ajili ya maendeleo ya watu, tushiriki sote hasa kwenye utatuzi wa changamoto za miundombinu. Kwa hiyo ni jukumu la Msingi la Wadau wa Elimu katika kila eneo na kila shule kuwa na utamaduni wa kukutana kwa pamoja kutafakari maendeleo ya shule kuona nini wao kama jamii wanaweza kufanya kuchangia utatuzi wa changamoto za kielimu zinazowakabili.

Kuhusu swala la chakula shuleni; Wazazi wanapaswa kufahamu wazi kuwa ni juukumu lao la kisheria kuwapatia watoto wao chakula cha mchana wawapo shuleni. Hivyo, ni wajibu wao kukaa pamoja na kuona namna nzuri wanavyoweza kuwapatia watoto wao chakula cha mchana wawapo shuleni ili waweze kujifunza kwa ufanisi. Jambo la msingi na la kuzingatia ni kuwa wakati wote wa kutekeleza wajibu wao wazazi wasiwahusishe wanafunzi na au utoaji wa chakula shuleni usiwe wa kibaguzi. Kama upo mpango wa chakula shuleni uliokubaliwa na wazazi wote basi wanafunzi wote wapate chakula bila kujali uwezo wa wazazi wao kuchangia chakula hicho. Utaratibu uwe wazi na uliokubaliwa na kupata vibali kutoka mamlaka husika.

Ndugu Wadu wa Elimu; leo tumekutana kutafakari yaliyopo na yaliyopita ili tupange yajayo. Ukiangalia maendeleo ya elimu katika wilaya yetu ni ya kuridhisha lakini zipo changamoto kama kutofanya

vizuri kama inavyopaswa kwa shule zetu. Kwa mfano ufaulu wa mitihani wa shule zetu unaweza kuuona na ufaulu wa jumla wa wilaya pia upo. Kwa ujumla ufaulu wetu kama alivyotuambia Mkurugenzi unahitaji juhudi Zaidi ili tuweze angalau kuwepo katika kumi bora za kitaifa katika mitihani yote. Hapa naomba Mkurugenzi wa Manispaa Mkakati wa dhati uwekwe kufuatilia na kusimamia ijifunzaji na ufundishaji shuleni ili wilaya yetu ifanye vizuri na kwa kuanzia tuingie kumi bora kitaifa. Haya yanawezekana ikiwa kila shule na kila Mdau utatimiza wajibu wake. Naomba tukikutana kwenye hafra kama hii mwaka 2018 cha kwanza itakuwa ni kujiuliza kuwa ni katika Mtihani upi wa kitaifa tumeingia kumi bora na upi hatukuingia na sababu za kutoingia zitapaswa kuainishwa.

Mwisho, nachukua fura hii kuwapongeza wote walifanikisha uendeshaji wa Wiki ya Elimu katika Wilaya ya Kinondoni ikiwemo Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Programu ya LANES, na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, pia Wadau wengine wa Elimu waliochangia katika uendeshaji wa Juma hilo ambao ni pamoja na Chemicotex, Oxford University Press, Education Publisher, Shule ya Sekondari Mbezi Beach,CRDB Kijitonyama, Jeshi la Wananchi wa Tanzania,Kituo cha Walimu Mwenge, Mwalimu Kiduma S. Mageni, NGOPSO, WOISO Original Product, Save the Children, Atlas Madale Schools na Coca Cola LTD, Nawashukuru sana kwa niaba ya Serikali kwani fedha mlizochangia zingeweza

kufanya kazi nyingine tofauti nahii, lakini mkachagua kuwezesha na kuongeza hamasa katika utoaji wa elimu katika Manispaa yetu. Mwenyezi Mungu awazidishie moyo wa kujitolea Zaidi. Aidha nawaalika Wadau wengine wenye nia njema kuendelea kujitokeza kwa wingi kuchangia maendeleo ya elimu katika wilaya yetu. Mwakani naimani tutafanya vizuri Zaidi ya hapo.

Nawapongeza pia Shule, Wanafunzi na Walimu wote ambao wamefika hapa leo na watapewa tuzo mbalimbali kutambua juhudi zao. Kazi kubwa mmefanya maana mlikuwa wengi mpaka ninyi kujitokeza si kazi rahisi. Kwa dhati kabisa nawapongeza sana. Leo mtapata zawadi mbalimbali kama zilivyoandaliwa. Wanafunzi watapa vitabu vya kiada, walimu watapata fedha taslimu na shule zitapata ngao mbalimbali.

Baada ya maelezo hayo niseme nawatakia hafra yenye mafanikio makubwa na sasa niko tayari kwa hatua iliyofuata

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA

MANYAMA MANGALU
NAIBU MEYA
MANISPAA YA KINONDONI